



**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO  
NA TEKNOLOJIA YA HABARI  
TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI  
TAARIFA KWA UMMA**



## **YAH: UMUHIMU WA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI**

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania (PDPC) inawakumbusha Wananchi na Taasisi zote za umma na binafsi kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya 2022.

Tume inawakumbusha wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi kuwa na wajibu wa kuhakikisha usalama na faragha ya taarifa za wateja wao kwa mujibu wa sheria. Ni muhimu kuchukua hatua za kuzuia uvujaji wa taarifa ili kuepuka kuvunja sheria na faragha za wateja.

Tume inaonya kuwa uvunjaji wa sheria ya faragha na taarifa binafsi utachukuliwa kwa uzito na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wahusika. Ni jukumu la kila mkusanyaji na mchakataji wa taarifa binafsi kuhakikisha taarifa zinalindwa dhidi ya ufikiaji usioidhinishwa na matumizi mabaya.

Kwa maelezo zaidi au kutoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa faragha, tafadhali wasiliana na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kupitia dawati la msaada kwa barua pepe [helpdesk@pdpc.go.tz](mailto:helpdesk@pdpc.go.tz) au simu namba +255718462536; +255744057652; +255736110505; +255615779070

Imetolewa leo Jumanne tarehe 11 Juni, 2024 na:

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi**

***“Faragha Yako Ni Wajibu Wetu”***

**Jengo la UCSAF, Barabara ya 10, S. L. P. 1105, Dodoma - Tanzania  
Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505,**

     @pdpc.tz  [www.pdpc.go.tz](http://www.pdpc.go.tz)